



Awamu ya 2 Mwaka wa 2

70 Eliya katika Mlima wa Karmeli

Kwa Biblia

1 Wafalme 18 :16—46

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba kuna Mungu mmoja tu. Tusiogope kuwa waaminifu kwa Mungu

Somo

Hakukuwa na mvua kwa karibu miaka mitatu. Halafu Mungu aliambia Eliya aende kwa Ahabu. Mungu alisema ataleta mvua kwa nchi.

Ahabu na watu waliabudu mungu wa uongo Baali. Eliya aliabudu Mungu wa kweli. Eliya aliambia mfalme Ahabu akusanye watu wote kwa Mlima wa Karmeli. Eliya alisema kwamba lazima hata manabii 450 wa Baali nao wakuje kwa Mlima wa Karmeli.



Mfalme Ahabu alisanya watu wote kwa Mlima wa Karmeli. Eliya alizungumza na watu, "Lazima muamue, nani ndiye Mungu wa kweli. Kama Bwana ndiye Mungu wa kweli, haya mmuabudu. Lakini kama Baali ndiye mungu wa kweli, basi mmuabudu."

Eliya aliwambia kwamba yeye ndiye nabii wa Mungu pekee. Lakini kuna manabii wa Baali 450. Eliya aliwambia atawaonyesha nani ndiye Mungu wa kweli.

Baali mungu wa uongo – sanamu ya kuchongwa

Maswali


1. Mungu wa uongo aliyeabudiwa na Ahabu na watu aliitwa nani?
2. Eliya aliambia Ahabu asanye watu wapi?
3. Manabii wa Baali walikuwa wangapi?
4. Eliya na manabii wa Baali walijenga nini?
5. Waliweka nini kwa madhabahu? Waliweka moto wowote?
6. Watu wangejua namna gani Mungu wa kweli?
7. Baali alituma moto kwa madhabahu yake?
8. Eliya alimwaga nini kwa madhabahu yake?
9. Mungu alituma nini kwa madhabahu ya Eliya?
10. Mungu alituma nini baada ya watu kumwamini?

Majibu

1. Mungu wa uongo aliitwa Baali.
2. Watu walikusanyika kwa Mlima wa Karmeli.
3. Kulikuwa na manabii 450 wa Baali.
4. Eliya alijengea Mungu madhabahu. Manabii 450 walijengea Baali madhabahu.
5. Waliweka ng'ombe dume kwa kila madhabahu. Hawakuweka moto.
6. Mungu wa kweli atatuma moto uchome ng'ombe.
7. La. Baali hakutuma moto.
8. Eliya alimwaga mapipa 12 ya maji juu ya madhabahu.
9. Mungu alituma moto uliochoma ng'ombe, madhabahu na maji yote.
10. Mungu alituma mvua kwa nchi.

Eliya aliwambia watu kwamba watachagua nani ndiye Mungu wa kweli. Eliya atajengea Mungu madhabahu na aweke juu yake ng'ombe dume. Lakini hataweka chini yake moto wowote. Manabii wa Baali nao watajenga madhabahu na waweke ng'ombe mwininge. Hawataweka chini yake moto. Eliya ataomba Mungu na manabii 450 wataomba Baali. Mungu atakayetuma moto ichome ng'ombe ndiye Mungu wa kweli. Watu walikubali kwamba hilo ndilo wazo mzuri.

Manabii 450 walijenga madhabahu ya Baali. Waliweka ng'ombe juu yake. Lakini hawa Manabii walipiga kelele kwa Baali asubuhi yote. Lakini hakukuwa na jibu. Manabii waliongeza sauti ya kelele. Walisema kwa kelele, "Baali, utusikie. Ee Baali, utujibu!"



Eliya aliwafanya dhihaka. Alisema, "Paza sauti juu! Labda Baali anazungumza. Ama labda analala kwa hivyo mnatakiwa mmuamshe! Manabii wa Baali walipiga kelele kwa sauti zaidi. "Baali! Baali! Tusikie na utujibu, Baali!" Manabii walicheza wakizunguka madhabahu. Walirukaruka juu na chini kwa madhabahu. Walijikatakata kwa visu. Mchana kutwa manabii wa Baali walipiga kelele. Lakini hakukuwa na jibu. Hakukuwa na moto kwa madhabahu yao.

Ilipofika jioni, Eliya aliambia watu, "Kuja hapa nilipo." Eliya alirekebisha madhabahu iliyokuwa imearibiwa. Eliya alichimba mfereji, akazungusha madhabahu. Eliya aliwambia walete maji na kujaza mapipa 12. Labda maji yalitoka kwa ziwa iliyokuwa karibu na Mlima wa Karmeli. Maji yalimwagwa juu ya madhabahu iliyokuwa na sadaka ya ng'ombe. Kila kitu kililowa maji. Mfereji ulijaa maji. Haikuwa rahisi moto uwake pale.

Eliya aliangalia juu mbinguni. Aliomba Mungu, "Bwana Mungu wa Ibrahim, Isaka na Yakobo, onyesha watu kwamba wewe ni Mungu wa kweli. Nisikie, Ee Bwana na unijibu. Onyesha watu kwamba wewe ni Bwana, Mungu wa Israeli."



Kulikuwa na mlipuko. Watu waliogopa. Moto ultoka kwa Mungu na ukachoma huyo ng'ombe. Huo moto ulichoma madhabahu. Ulichoma na kukausha hayo maji yaliyokuwa kwa mfereji.

Watu waliogopa. Walianguka chini. Walilia na kusema, "Bwana, Yeye ni Mungu! Bwana, Yeye ni Mungu." Eliya alisema, "Chukua manabii wa Baali. Msimwaje hata mmoja aende. Waue wote." Watu waliua manabii wa Baali wote.

Halafu Eliya akaomba Mungu alete mvua kwa nchi. Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mitatu mvua ilinyesha. Njaa iliisha. Mungu alionyesha watu kwamba Yeye ni Mungu wa kweli. Hakuna Mungu mwininge.